BARAZA LA TAIFA LA UJENZI
(NATIONAL CONSTRUCTION COUNCIL)

Mansfield Street, P.O. Box 70039, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255-22-2131321, +255-22-2135553, +255-22-2110869, Fax: +255-22-2118887 E-mail: ncc@ncc.or.tz, Website: www.ncc.or.tz
(Currently temporarily relocated to 9th Floor of Office Accommodation Scheme Building Azikiwe Street-Dar es salaam)

MADHUMUNI

Baraza la Taifa la Ujenzi ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge namba 20 ya mwaka 1979 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2008. **("National Construction Council Act, CAP 162, R.E. 2008")**. Baraza lilianzishwa ili kusimamia maendeleo ya sekta ya ujenzi.

DIRA

Kutoa uongozi mkakati unaolenga katika maendeleo ya sekta ya ujenzi kwa kutilia mkazo ukuzaji wa uwezo wa ndani.

MAJUKUMU YA BARAZA

Baraza ni kitovu cha uratibu wa sekta kwa taasisi zinazoshughulika na ujenzi ili kuleta umoja, uwiano na ushirikiano katika utendaji ndani ya sekta ya ujenzi. Hususani majukumu ya Baraza ni kama ifuatavyo:

- Kusimamia na kuongoza juhudi za kukuza na kuendeleza sekta ya ujenzi nchini Tanzania kwa kuzingatia ukuzaji wa uwezo wa ndani ya nchi ili kwenda sambamba na maendeleo na ushindani wa kimataifa;
- Kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu sekta ya ujenzi na kutayarisha mapendekezo, maelekezo na utekelezaji wake;
- Kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau wa sekta ya ujenzi;
- Kukuza na kuratibu mafunzo bora kwa watu wanaojihusisha au watakaojihusisha na sekta ya ujenzi;
- Kukuza, kuendesha na kuratibu utafiti katika masuala yanayohusiana na sekta ya ujenzi;
- Kutayarisha na kutunza orodha ya miradi na kuhamasisha utunzaji wa uenezaji wa taarifa zinazohusiana na sekta ya ujenzi;
- Kusimamia na kuratibu maendeleo na utekelezaji wa viwango, kanuni na miongozo ya kiufundi inayohusiana na sekta ya ujenzi;
- Kukuza na kuhimiza matumizi ya teknolojia za kisasa na utendaji endelevu, katika sekta ya ujenzi;
- Kukuza na kuanzisha makongamano yanayolenga katika ushirikiano na majadiliano katika masuala yanayohusu sekta ya ujenzi;
- Kusimamia na kutathimini mwenendo wa utendaji wa sekta ya ujenzi;
- Kuanzisha na kusimamia mfuko wa fedha kwa ajili ya mafunzo ya wadau wa sekta ya ujenzi;
- Kukuza na kusimamia ubora wa kazi za ujenzi ikijumuisha utoaji wa huduma ya ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi;
- Kuendeleza teknolojia za ujenzi unaolenga katika mbinu za utunzaji mazingira na kuzingatia afya na usalama;

- Kuendeleza utoaji huduma nje ya mipaka ya nchi kwa kuzingatia ubora katika sekta ya ujenzi;
- Kusimamia utatuzi wa migogoro katika sekta ya ujenzi.

HUDUMA

Huduma kuu zitolewazo na Baraza zinajumuisha uratibu wa sekta, ushauri, usuluhishi wa migogoro, mafunzo, ukaguzi wa kiufundi, utafiti uchapishaji na usambazaji wa taarifa na ushirikiano kikanda na kimataifa.

URATIBU WA SEKTA

Sera na Mikakati

Baraza limehusika katika uratibu na uundaji wa sera na mikakati mbalimbali kwa ajili ya sekta ya ujenzi kama ifuatavyo:

- Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi wa Mwaka 1990;
- Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003;
- Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Ujenzi ya mwaka 2006;
- Mwongozo wa manunuzi yanayohusisha utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi wa mwaka 2008;
- Rasimu ya Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ya mwaka 2008.

Vyama na bodi za usajili

Baraza lilihamasisha uundwaji wa bodi za usajili na vyama vya wadau wa sekta ya ujenzi; ikiwa ni pamoja na:

- Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wakadiriaji Majenzi - **(Architects and Quantity Surveyors Registration Board);**
- Bodi ya Usajili wa Makandarasi - **(Contractors Registration Board);**
- Bodi ya Usajili wa Wahandisi - **(Engineers Registration Board**);
- Chama cha Wabunifu wa Majenzi - **(Architects Association of Tanzania);**
- Chama cha Wahandisi Washauri - **(Association of Consulting Engineers Tanzania);**
- Chama cha Makandarasi Wahandisi Ujenzi - **(Tanzania Civil Engineering Contractors Association);**
- Chama cha Barabara - **(Tanzania Roads Association);**
- Taasisi ya Usuluhishi na Migogoro - **(Tanzania Institute of Arbitrators);**
- Taasisi ya Wakadiriaji Majenzi - **(Tanzania Institute of Quantity Surveyors);**
- Chama cha Wajenzi wa Sekta isiyo Rasmi - **(Tanzania Association of informal Construction Workers);**
- Mfuko wa Maendeleo wa Sekta ya Ujenzi - **(Construction Industry Development Fund).**

Pia Baraza limeshiriki katika uanzishwaji wa vyama vifuatavyo:

- Chama cha Washauri - **(Tanzania Association of Consultants);**
- Chama cha Wadau wa Sekta Binafsi - **(Tanzania Private Sector Foundation);**
- Taasisi ya Utawala Bora - **(Tanzania Institute of Corporate Governance).**

Makongamano ya sekta ya ujenzi

Kuanzia mwaka 2001 Baraza limekuwa likiandaa makongamano ya sekta ya ujenzi mara moja kila miaka miwili. Madhumuni ya makongamano ya sekta ya ujenzi ni

kusaidia upangaji, uratibu pamoja na kuboresha maendeleo ya sekta ya ujenzi kwa kuzingatia yafuatayo:

- Dira, malengo na mikakati ya maendeleo ya sekta ya ujenzi;
- Mikakati ya kukuza uwezo ili kuboresha utendaji katika sekta;
- Ukuaji wa sekta ili kukabiliana na ushindani wa Kimataifa;
- Matumizi ya teknolojia inayofaa na ya kisasa;
- Uhusiano wa kitaifa na kimataifa.

HUDUMA ZA USHAURI

Baraza linashughulika na kutoa ushauri wa kiufundi katika mambo mbalimbali yanayohusu sekta ya ujenzi; ikiwa ni pamoja na bei, ya vifaa vya ujenzi gharama za ujenzi, mabadiliko ya bei ya vifaa vya ujenzi, madai, teknolojia, mahitaji ya mafunzo, na utayarishaji na usimamizi wa miradi na ufafanuzi wa mikataba.

USULUHISHI WA MIGOGORO

Tangu mwaka 1982 Baraza limekuwa likijihusisha na usuluhishi wa migogoro ya ujenzi. Baraza lina orodha ya wasuluhishi ambao husajiliwa kutokana na sifa zao ambao wanaweza kutumiwa na wateja kwa kuchagua wenyewe. Aidha utatuzi wa migogoro hufuata kanuni za usuluhishi ambazo huchapishwa na Baraza.

MAFUNZO

Mafunzo ni muhimu sana katika kukuza uwezo wa wadau wa sekta ya ujenzi. Mafunzo yanasaidia utendaji bora wa kazi ambao ni muhimu katika kukuza na kuongeza ubora na tija, pia kuwezesha kukabiliana na ushindani na kuleta thamani halisi kwa fedha zilizotumika katika miradi ya ujenzi. Baraza linaendesha mafunzo kwa njia ya vitendo katika nyanja mbalimbali zinazohusiana na ujenzi zikijumuisha: manunuzi, usimamizi wa mikataba, usimamizi wa miradi, ukadiriaji wa gharama za ujenzi, sheria zinazohusiana na mikataba ya ujenzi, ukaguzi wa kiufundi, usuluhishi wa migogoro, menejimenti ya madai, mafunzo kwa wadau, ubia kati ya sekta binafsi na ya umma, ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi, matengenezo ya majengo pamoja na matumizi ya komputa katika ukadiriaji wa bei za majenzi. Mafunzo pia yanatolewa kwa watu wenye mahitaji maalum kufuatana na mahitaji yatakayowasilishwa.

Tangu mwaka 2000 Baraza limefundisha wadau wapatao 3252 wakijumuisha wahasibu, wabunifu majengo, wahandisi, wasimamizi wa majenzi, mawakala wa bima, wanasheria, wakadiriaji majenzi, wafanyakazi wa serikali za mitaa, madiwani, maafisa ugavi, wahakiki mali, wathamini, wakandarasi na mafundi mchundo

UKAGUZI WA KIUFUNDI

Madhumuni ya kufanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi ni kuwasaidia wawekezaji kupata maelezo kuhusu mwenendo na utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na mapungufu yaliyopo, na utatuzi wake. Ukaguzi unaweza kufanyika katika hatua yeyote ya mradi ikiwa ni pamoja na matayarisho ya utekelezaji, wakati wa utekelezaji na baada ya mradi kutekelezwa. Baraza limekuwa likitoa huduma hii kwa serikali na taasisi zake na sekta binafsi, kwa mfano, tangu mwaka 2005, Baraza limekuwa likikagua kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, miradi mikubwa inayogharimiwa na serikali kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

MWAKA	2005	2006	2007	2008	2009
Idadi ya Miradi	26	40	24	24	49
Thamani Shilingi (Bilioni)	399	386	500	750	762

UTAFITI

Kazi za utafiti zinazolenga katika kutambua matatizo mbalimbali na ufumbuzi wake yanayohusiana na sekta ya ujenzi kwa ujumla, ni mojawapo ya shughuli za Baraza. Tafiti zilizowahi kufanywa na Baraza ni pamoja na tafiti kuhusu uanzishwaji wa mfuko maalum wa kuwasaidia wadau wa sekta ya ujenzi kupata mahali pa kukopa fedha au kupata dhamana kwa ajili ya miradi ya ujenzi; mahitaji ya rasilimali watu katika sekta ya ujenzi nchini Tanzania; mahitaji ya mafunzo kwa washauri na wakandarasi wa miundombinu ya umwagiliaji katika kilimo; uanzishwaji wa mfuko endelevu wa mafunzo kwa wadau wa sekta ya ujenzi nchini Tanzania; mapendekezo ya kuhuishwa sheria iliyoanzisha Baraza la Taifa la Ujenzi; utafiti kuhusu namna ya kuliwezesha kifedha, Baraza la Taifa la Ujenzi ili tuweze kutekeleza majukumu yake bila matatizo; utafiti kuhusu utendaji kazi katika miradi mikubwa ya ujenzi kwa kuzingatia ushiriki wa sekta ya umma na binafsi; utafiti kuhusu kitengo cha makontena bandarini; utafiti kuhusu wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi katika ujenzi.

Tafiti nyingine zilizofanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Eindhoven cha Uholanzi kupitia wanafunzi wao waliokuwa wanachukua shahada ya uzamili (**Master of Science degree)** zinajumuisha matumizi ya teknolojia ya mianzi nchini Tanzania; uwekezaji katika ujenzi wa nyumba nchini Tanzania; wingi na ubora wa nyumba nchini Tanzania; matumizi ya chokaa na jasi katika sekta ya ujenzi; matumizi ya teknolojia ya mianzi katika ujenzi wa nyumba, na uzalishaji wa saruji kwa kutumia viwanda vidogo hapa nchini.

MACHAPISHO YA KIUFUNDI NA UTOAJI TAARIFA

Baraza limekuwa likikusanya na kusambaza taarifa muhimu katika sekta ya ujenzi. Aidha, Baraza limechapisha miongozo ya kiufundi na linaweka hazina ya taarifa na kuna maktaba yenye vitabu na majarida yanayohusu sekta ya ujenzi. Baadhi ya machapisho yaliyopo ni pamoja na:

- Kanuni za usuluhishi wa migogoro ya ujenzi - **(Arbitration Rules);**
- Mwongozo wa mabadiliko ya bei - **(Price Fluctuation Formula Indices);**
- Mkataba wa ujenzi wa majengo - **(Agreement and Schedule of Condition of Building Contract - with Quantities);**
- Mkataba mdogo wa ujenzi wa majengo - **(Agreement and Schedule of Condition of Building Subcontract - with Quantities);**
- Mwongozo wa vifaa vya ujenzi - **(Directory of Construction Materials);**
- Takwimu muhimu za sekta ya ujenzi – **(Basic Statistical Data for Construction Sector);**
- Miongozo 14 ya kiufundi kuhusu nyanja mbalimbali katika sekta ya ujenzi – **(Technical Guidelines);**
- Jarida **(Construction Business)** linalochapishwa kila baada ya miezi miwili.

USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

Baraza limekuwa likishiriki katika taasisi za kimataifa kwa mfano chama cha barabara cha kimataifa **(World Road Association – PIARC)** taasisi ya kivumbuzi na utafiti katika sekta ya ujenzi **(International Council for Research and Innovation in Building and Construction).** Aidha kwa sasa hivi Baraza linaratibu shughuli za mradi unaohamasisha uwajibikaji na uwazi katika sekta ya ujenzi **(Construction Industry**

Transparency Initiative-CoST). Mradi huu unalenga kusaidia katika kupambana na rushwa katika sekta ya ujenzi na kwa sasa unahusisha nchi zifuatazo: Ethiopia, Malawi, Philippines, Tanzania, Uingereza (UK), Vietnam na Zambia na unafadhiliwa na Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID).

MFUMO WA BARAZA

Baraza lina Wajumbe 15 akiwepo mwenyekiti wake. Wajumbe wanateuliwa na Waziri anayeshughulika na masuala ya ujenzi na wanatoka katika taasisi za umma na binafsi. Uwakilishi toka taasisi za umma ni kutoka katika wizara ya miundombinu, ardhi na maendeleo ya makazi, maji, fedha, sayansi na teknolojia, na taasisi za elimu ya juu. Sekta binafsi zinawakilishwa na taasisi za makandarasi, wabunifu majenzi, wahandisi, wakadiriaji majenzi na watengenezaji na wasambazaji wa mitambo na vifaa vya ujenzi, na taasisi inayohusika na sekta binafsi. **(Tanzania Private Sector Foundation).** Mwenyekiti anateuliwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Katibu wa Baraza ni Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Ujenzi.

WAFANYAKAZI WA BARAZA

Wafanyakazi wa Baraza wanajumuisha wahandisi, wakadiriaji majenzi, wanasayansi wa habari na wengine wa fani za usaidizi.

WATEJA WA BARAZA

Wateja wa Baraza wanajumuisha wadau wote wa sekta ya ujenzi yaani serikali, taasisi za serikali, mashirika ya maendeleo ya nje na ndani ya nchi, taasisi za uendelezaji na usimamizi na vyama vya kitaaluma, makandarasi, washauri na sekta binafsi.

CHANGAMOTO

Baraza likiwa kama kitovu cha kuunganisha masuala ya sekta linahitaji rasilimali za kutosha ili kutimiza majukumu yake ya kusimamia na kuratibu maendeleo ya sekta ya ujenzi, na kwa ajili ya ukuaji wake na kuhimili ushindani wa kimataifa.